Ombi la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Arusha (Arusha Urban Water Supply and Sewerage Authority - AUWSA) la kurekebisha Bei ya Huduma ya Majisafi na Majitaka lililowasilishwa Tarehe 3 Septemba 2008.

(TR-W-08-015)

AGIZO Na. 09-10

Tarehe 3 Septemba, 2008 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji ("EWURA") ilipokea ombi la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Arusha ("AUWSA") la kurekebisha bei za huduma ya majisafi na majitaka. Katika ombi hilo, AUWSA iliomba kuongeza bei ya majisafi hadi asilimia 30.4 kwa wateja waliofungiwa dira. AUWSA iliomba pia kuongeza bei ya majitaka kwa kati ya asilimia 12.5 na asilimia 16. Bei na gharama mpya ziliombwa zianze kutumika kuanzia tarehe 1 Januari 2009. Wakati wakufanya tathmini ya pendekezo hili, AUWSA walitakiwa walete bajeti ya mwaka wa fedha wa 2009/2010 ambayo bei na gharama za maji zilizoombwa zitatumika. Hata hivyo, AUWSA waliomba kuleta bajeti hiyo mwanzoni mwa mwezi wa tano mwaka 2009 baada ya bodi yao kukaa na kupitisha bajeti hiyo. AUWSA walipoleta bajeti yao ya mwaka 2009/10, waliomba pia kuwa bei na gharama walizioomba sasa zianze kutumika kuanzia tarehe 1 Julai 2009.

Pendekezo la bei la AUWSA linalenga kuiwezesha AUWSA kumudu ongezeko la gharama na kuweza kulipia gharama zote za uendeshaji.

Sheria ya EWURA, "Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act" (Sura ya 414)", imeipa EWURA uwezo wa kisheria wa kudhibiti marekebisho ya bei katika sekta ya majisafi na majitaka. Katika kutathmini maombi ya AUWSA, EWURA imezingatia, pamoja na mambo mengine, taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na AUWSA kama zinavyoelekezwa na mwongozo wa EWURA wa maombi ya

kurekebisha bei, taarifa za nyongeza kwa ajili ya kutoa ufafanuzi, hoja na fafanuzi mbalimbali kutoka kwa wadau.

Mkutano wa taftishi ulifanyika tarehe 30 Oktoba 2008 katika ukumbi wa Manispaa mjini Arusha ili kupata maoni kuhusu uhalali wa ombi hilo la ongezeko la bei za majisafi na majikata.

Katika mkutano huo, wadau mbalimbali miongoni mwao wakiwa in Baraza la Watumiaji Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (CCC), Baraza la Ushauri la Serikali (GCC), na wananchi wa Arusha walipewa fursa ya kutoa maoni yao kuhusu ombi la AUWSA la kuongeza bei ya huduma zake. Mabaraza yote mawili yalikuwa na hoja kuhusu gharama kubwa za utawala pamoja na uendeshaji zinazosababisha ombi kubwa la kuongeza bei ya majisafi kwa asilimia 13. Wananchi walikuwa na hoja ya ada kubwa ya kuunganishiwa maji licha ya kununua mabomba na viungio. Wananchi walitoa malamiko yao kuhusu bei kubwa wanayotoza kwenye Maghati.

Uchambuzi wa makisio ya mahitaji ya mapato umeonyesha kuwa, AUWSA ilipaswa kuomba nyongeza ya bei ya majisafi ya asilimia 0 hadi 13.04 badala ya asilimia 0 hadi 30.4 ambayo ilipatikana kutokana na makisio ya mapato na matumizi katika Mpango Mkakati wa AUWSA wa mwaka 2006 hadi 2011.

Kufuatia kukamilika kwa taftishi, EWURA imefikia uamuzi kwamba ombi la ongezeko la bei lina mantiki na ni halali isipokuwa makisio makubwa ya gharama za uwekezaji ambayo yalikuwa hayaendani na makubaliano ya kiutendaji ambapo AUWSA alitakiwa kuwekeza asilimia 18 tu ya mapato yake.

Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha tarehe 25 Juni 2009 ilijadili ombi la AUWSA na kutoa maamuzi yafuatayo:

1.0 Bodi imeidhinisha ongezeko la asilimia kati ya 0 hadi 13.04 ya bei ya majisafi kwa wateja waliofungiwa dira. Aidha, Bodi imeidhinisha bei ya majitaka iongezeke kwa kati ya asilimia 12.5% na asilimi 16. Bei zilizoidhinishwa zinaonyeshwa kwenye jedwali Na 1 na 2 hapa chini.

Jedwali Na. 1: Bei za Majisafi (kwa wateja waliofungiwa dira)

Na.	Kundi la wateja	Bei ya Sasa		Bei iliyoombwa		Bei iliyoidhinishwa	
		Kiwango cha Matumizi (Mita za Ujazo	TZS/Mita ya Ujazo	Kiwango cha Matumizi (Mita za Ujazo	TZS/Mita ya Ujazo	Kiwango cha Matumizi (Mita za Ujazo	TZS/Mita ya Ujazo
1.	Majumbani	0-5	300	0-5	350	0-5	335
		5-15	350	5-15	400	5-15	395
		>15	400	>15	450	>15	450
2.	Taasisi	0-5	300	0-5	350	0-5	335
		5-15	325	5-15	375	5-15	365
		>15	350	>15	400	>15	395
3.	Biashara	0-5	345	0-5	450	0-5	390
		5-11	435	5-11	475	5-11	475
		>11	515	>11	550	>11	550
4.	Viwanda	0-5	500	0-5	550	0-5	550
		5-10	550	5-10	600	5-10	600
		>10	600	>10	650	>10	650
5.	Maghati		150		150		150
6.	Viwanda vya kutengeneza maji		3,400		4,000		3,850

Jedwali Na.2: Bei za Majitaka

Kundi la wateja	Bei ya Sasa (TZS kwa Meta ya Ujazo)	Bei Iliyoombwa (TZS kwa Meta ya Ujazo)	Bei Iliyoidhinishwa (TZS kwa Meta ya Ujazo)
Majumbani	95	110	110
Taasisi	95	110	110
Biashara	120	130	130
Viwanda	150	170	170
Viwanda vya kutengeneza maji	150	170	170

2.0 Ifakapo tarehe 30 Septemba 2009 au kabla ya hapo, AUWSA inatakiwa iwe imewasilisha kwa EWURA ripoti ya utekelezaji wa zoezi la kurekebisha takwimu na kumbukumbu zao kuhusiana na madeni sugu.

3.0 AUWSA inatakiwa ihakikishe kuwa watumiaji wa Maghati wanalipa bei ya majisafi kama ilivyopitishwa na EWURA.

4.0 Ifikapo tarehe 30 Septemba 2010 au kabla ya hapo, AUWSA inatakiwa iwe imewasilisha kwa EWURA ripoti ya utekelezaji wa miradi ya uwekezaji na mchanganuo wa gharama zilizotengwa kwa ajili ya uchakavu wa mitambo katika bajeti ya mwaka 2009/10.

5.0 AUWSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji wake kwa mujibu wa mwongozo wa EWURA. Taarifa hizo zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa AUWSA ikilinganishwa na asasi zingine za utoaji wa huduma za majisafi na majitaka na uboreshaji wa huduma zake. EWURA itazingatia matokeo ya tathmini hiyo katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na AUWSA katika siku zijazo. Inasisitizwa kuwa, AUWSA itaboresha taarifa zote zinazowasilishwa EWURA kila mwezi.

Agizo hili litaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai 2009.

Simon F. Sayore
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
EWURA

Haruna Masebu
Mkurugenzi Mkuu
EWURA

Dar - es – Salaam 25 Juni 2009